Magesa awataka walimu kushikamana Uk. 4

Sauti ya Mwalimu

CHAMA CHA WALIMU TANZANIA
CWT
WAJIBU NA HAKI

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

Toleo Na.006 Agosti - Septemba 30, 2022

# Maslahi ya Walimu nchini ndio kipaumbele chetu- Mathamani

- Awataka walimu wasiyumbishwe
- Asisitiza CWT itaendelea kuwapigania

Ameyasema hayo wakati akiongea na walimu nchini kupitia Kongamano la SOHITCO lililofanyika Mkoani Iringa na kukutanisha wajumbe kutoka Mikoa ya Katavi,Rukwa,Njombe,Songwe,Mbeya na Iringa Pamoja na walimu wa Manispaa ya Iringa. Habari kamili Uk.1





# Chama Cha Walimu Tanzania champongeza Rais Samia



Habari kamili Uk.3



# Njia ya majadiliano imetupa manufaa asema Maganga

Kaimu Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Mwalimu Maganga Japhet amewaambia walimu nchini kuwa njia waliyochagua ya kukaa meza moja na Serikali na kujadiliana kuhakikisha changamoto zinazomkabili mwalimu zinatatuliwa imekuwa na manufaa

Habari kamili Uk.2

# Maslahi ya Walimu nchini ndio kipaumbele chetu



***Na Mwandishi wetu***

Kaimu rais wa Chama Cha Walimu Tanzanian (CWT) Mwalimu Dinah Mathamani (Pichani) amewahakikishia walimu nchini kuwa CWT itaendelea kutetea maslahi yao kama ilivyokuwa hapo awali na wasiyumbishwe na manenno ya watu kwamba kwa sasa haifanyi kazi hiyo. Ameyasema hayo wakati akiongea na walimu nchini kupitia Kongamano la SOHITCO lililofanyika Mkoani Iringa na kukutanisha wajumbe kutoka Mikoa ya Katavi,Rukwa,Njombe,Songwe, Mbeya na Iringa Pamoja na walimu wa Manispaa ya Iringa.

"CWT ni chama cha wafanyakazi nchini na lengo letu kubwa ni kuhakikisha maslahi ya Mwalimu tunayetetea na ndio maana kila siku tumekuwa tukikutana na viongozi wa Serikali kuhakikisha hilo linatekelezwa." amesema Mathamani.

Aidha amewataka walimu kuendelea kukipigania na kukilinda Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) kwani ndio chama pekee kwa sasa kinachomwakilisha mwalimu katika meza ya majadiliano yote yanayohusu maslahi ya mwalimu nchini Tanzania.

Sambamba na hilo Mathamani amesema uongozi uko imara na unaendelea kutimiza majukumu yake ya kila siku na unawaomba wanachama nao kuwa imara katika kipindi hiki chama kinapoelekea katika mikutano mikuu ya kikatiba. Kongamano la SOHITCO limefanyika Mkoani Iringa kwa mara ya pili na lengo lake kubwa ni kuwakutanisha viongozi na wanachama kujadili changamoto hizo na njia mbalimbali wanazozitumia katika kuzitatua ambapo Mwalimu Mathamani alifunga Kongamano hilo lililofanyika kwa la siku tatu.



# Njia ya majadiliano imetupa manufaa



Kaimu Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania(CWT) Mwalimu Maganga Japhet (Pichani) amewaambia walimu nchini kuwa njia waliyochagua ya kukaa meza moja na Serikali na kujadiliana kuhakikisha changamoto zinazomkabili mwalimu zinatatuliwa imekuwa na manufaa makubwa kuliko watu wanavyodhani.

Ameyasema hayo wakati akiongea na walimu wa Manispaa ya Iringa kwenye Kongamano la SOHITCO lililokutanisha viongozi na wanachama wa Chama Cha Walimu Tanzania katika ukumbi wa Kichangani Mkoani mkoani Iringa.

"Tumeamua kuchagua njia ya majadiliano ya mezani kama njia bora kabisa ya kudai haki na maslahi ya walimu, na tunaishukuru Serikali hii sikivu ya mama Samia Suluhu Hassan imekuwa ikitusikiliza na imeendelea kutatua changamoto zetu" amesema Maganga.

Aidha ameongeza kwa kutumia njia hiyo kumekuwa na mawasiliano ya karibu na Serikali na kipekee wanamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ambaye amewafungulia milango ya kutatua changamoto zilizopo. Maganga amesisitiza pia kupitia njia hiyo wameona Serikali imetangaza ajira za walimu 9800 huku pia ujenzi wa miundombinu ya madarasa zaidi ya elfu kumi na tano pamoja na kundi kubwa la walimu kwa miaka hii miwili ya uongozi wake wamepandishwa madaraja. Sambamba na hilo Maganga amesisitiza CWT wataendelea kuwatetea walimu nchini na kuhakikisha changamoto mbalimbali zinatatuliwa ili kuhakikisha maslahi ya mwalimu yanakuwa bora.

**Bodi ya Uhariri**

Mhariri Mkuu Mtendaji
Mwl. Maganga M. Japhet

Mhariri Mkuu Msaidizi
Neema Ezekia

Mhariri
Bathromeo C. Chilwa

Msanifu kurasa
Adam Masoud

Msambazaji
Irene Mrabu

Msimamizi
Charles Mbughuni

Mchapaji
Ansilla Protas

*CHAMA CHA WALIMU TANZANIA*
*S.L.P 3077 Dodoma. Barua pepe:info@ttu.or.tz*
*Tovuti: www.ttu.or.tz*



# CWT champongeza Rais Samia





*Rais Samia Suluhu Hassan*

***Na Mwandishi wetu Iringa.***

Kaimu rais wa Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) Mwalimu Dinah Mathamani (Pichani) kwa niaba ya viongozi wenzake wa Chama Cha Walimu amempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwa karibu na walimu nchini hasa baada ya kuhakikisha anatatua changamoto ya miundombinu ya madarasa, upandaji wa vyeo, mishahara na ajira mpya za walimu kwa kipindi kifupi cha uongozi wake.

Akiongea na walimu wakati wa kufunga Kongamano la SOHITCO kutoka Mikoa sita ya nyanda za juu kusini ya Katavi,Rukwa,Songwe,Mbeya,Njombe na Iringa, Mwalimu Mathamani amesema, “Kwa kipindi hiki kifupi tumeona ni kwa namna gani Rais anatupenda na ameendelea kututendea makubwa sisi walimu, na huu ndio wakati sahihi ambao wanachama wote hasa walimu kuja pamoja na kushikamana kuhakikisha hatumuangushi Rais kwa kufanya kazi kwa bidii na kutimiza wajibu wetu”. Aidha Mathamani amewaahidi walimu ushirikiano bora kwa kipindi hiki anachokaimu nafasi hiyo na kuwaomba walimu waendelee kushirikiana na viongozi kuhakikisha Chama Cha Walimu Tanzania kinasonga mbele na bila kuathiri malengo yake ya kutetea na kulinda maslahi ya walimu nchini.

Mbali na hilo amewaahidi walimu kuendeleza mazuri yote yaliyoanzishwa na watangulizi wake na atashirikiana na viongozi wenzake kuhakikisha maslahi ya walimu yanatetewa pamoja na kulinda hadhi na taaluma ya ualimu nchini. Katika kuhakikisha CWT inasonga mbele Mwalimu Mathamani pia amewataka walimu kufanya kazi kwa bidii na kuonyesha uzalendo katika kutimiza majukumu yao ya kila siku na kuwaahidi Chama kipo imara na kitaendelea kuwa imara.

# Magesa awataka walimu kushikamana



Kaimu mwekahazina wa Taifa wa Chama Cha Walimu Tanzania CWT Mwalimu Protas Magesa amewataka walimu nchini kushikamana na kukiamini Chama cha Walimu Tanzania (CWT) katika kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili walimu ikiwa ndio taasisi pekee inayowawakilisha walimu katika kutetea maslahi yao nchini. Ameongea hayo wakati wa ufunguzi wa Kongamano la SOHITCO lililojumuisha Mikoa sita ya Mbeya,Njombe,Songwe,Rukwa,Katavi na Iringa ambapo zaidi ya washiririki 270 ni walimu “Walimu tushikamane katika kupigania maslahi yetu na taasisi hii ndio itakayotufikisha katika malengo tunayoyatarajia kwani kwa takribani miaka 30 sasa CWT imefanya mambo makubwa hivyo niwaombe walimu tuilinde taasisi hii na tusikubali watu wabaya wakaingia na kuiharibu.” Aidha Magesa ameongeza na kusema CWT imekuwa ikipambania sana maslahi ya walimu na sisi viongozi tutaendelea kushikanama na nyie ili kutatua changamoto mbalimbali zinazotukabili. Akimkaribisha mgeni rasmi Mwalimu Stanslaus Mhongole Mwenyekiti wa CWT Mkoa Iringa, ameushukuru uongozi wa Mkoa wa Iringa kwa kuendelea kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili walimu na kusisitiza changamoto nyingi zilizoorodheshwa katika risala yao wanaomba zitatuliwe. Kongamano hili la Mikoa sita limefanyika kwa siku tatu kuanzia tarehe 13 hadi 15 Julai ambapo lilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) na Serikali ambapo mada mbalimbali ziliwasilishwa na lilifungwa na Kaimu rais wa CWT Mwalimu Dinah Mathamani ambaye aliwasihi walimu kuendelea kukiamini chama chao kwani ndio mkombozi wao.



# Kamati ya Ujenzi CWT yatarajia makubwa

Kamati ndogo ya Ujenzi ya Kamati ya Utendaji ya Taifa ya Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) imesema inatarajia kasi ya umaliziaji wa majengo matano ya ofisi za Mikoa ya Simiyu,Geita,Katavi,Songwe na Njombe itakuwa kubwa kwa kipindi kifupi na Mikoa husika itahamia katika majengo hayo.

Akiongea kwa niaba ya wajumbe wa Kamati, Naibu Katibu Mkuu wa CWT na Mwenyekiti wa Kamati hiyo mwalimu Maganga M.Japhet amesema tayari Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) kimeweka fedha kwenye akaunti ya Mkandarasi SUMA JKT kwa makubaliano waliyokubaliana ili kukamilisha mradi huo kwa haraka.

“Kama tulivyokubaliana kwenye kikao chetu, nikuombe mkandarasi kuongeza nguvu ya kukusanya vifaa vya ujenzi na wafanyakazi kufika eneo la ujenzi mapema iwezekanavyo kwani tunatamani na tunahitaji kuyatumia majengo haya na ukiangalia ni muda mrefu sasa umepita hayajafunguliwa ”Amesema Maganga

Maganga amesisitiza kuwa ujenzi huo ulikuwa na matarajio ya kukamilika mapema lakini kutokana na sababau mbalimbali umechelewa kukamilika na uongozi wa CWT uliamua kukaa na mkandarasi na kupitia mkataba wao na baada ya makubaliano ya pande zote wameanza kuweka kiasi cha fedha walichokubaliana na mkandarasi ili kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati.

Kwa niaba ya mkandarasi anayejenga majengo hayo Kapteni Enock Charles amesema wao kama SUMA JKT wako tayari kwenda na kasi ya CWT kuhakikisha majengo hayo yanakamilika mapema na ameahidi baada ya miezi miwili watakuwa na neno la kusema hasa katika umaliziaji wa majengo kama ya Geita,Njombe na Simiyu ambayo yako nyuma ukilinganisha na Majengo ya Mikoa ya Katavi na Songwe.

Aidha Katibu wa Kamati hiyo Mwalimu Nashon Amos amesema ujenzi huo ulianza mwaka 2016/2017 kwa lengo la kusogeza huduma kwa wanachama wao na Kamati ya ujenzi wameona maendeleo hayo na wamefurahishwa na hatua iliyofikiwa kwa baadhi ya majengo na wamewaahidi walimu katika Mikoa hiyo ifikapo Disemba mwaka huu watakuwa na neno la kusema juu ya ujenzi huo.

Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) kiliamua kujenga majengo hayo kwa lengo la kusogeza huduma kwa wanachama wake kwa mikoa Mitano ya Geita,Simiyu,Katavi,Njombe na Songwe ambayo ilikuwa haina majengo hya ofisi na tayari mkandarasi yuko eneo la kazi kuhakikisha kazi hiyo inakamilika kwa wakati.





# Benki ya Mwalimu ilivyonogesha Maonesho ya 46 ya Biashara



Mkuu wa Kitengo Cha Ukuzaji Biashara na Masoko wa Benki ya Mwalimu (MCB), Bi.Leticia Ndongole akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) katika Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa yaliyofanyika jijini Dar es Salaam






Wafanyakazi wa Mwalimu Benki wakiwa katika picha ya pamoja kwenye banda lao la Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa.









Kwa habari mbalimbali zinazohusu Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) tafadhali tembelea kurasa zetu za mitandao ya kijamii

**cwt_tz** **chama__cha__walimu__tanzania** **chama cha walimu tanzania**

# CWT kimefanya makubwa nchini asema Chinahova



Katibu wa Chama cha Walimu Mkoani Iringa mwalimu Hamis Chinahova (Pichani) amesema Chama Cha Walimu Tanzania kimefanya mambo makubwa na ya kukumbukwa katika kuendeleza mustakabali wa taaluma na hadhi ya ualimu nchini. Chinahova ameyasema hayo wakati akiongea na waandishi wa habari ofisini kwake na kusema tangu kuanzishwa kwa chama hicho mwaka 1993 wamepata mafanikio kwenye maeneo mengi.

Alitaja baadhi ya mafanikio hayo kama vile kushawishi Serikali katika kutoa ajira kwa walimu kuanzia ngazi ya awali, msingi,sekondari na vyuo. Kutoa elimu kwa wanachama na viongozi, kuchapisha na kusambaza maandiko yanahusu kazi/fani ya ualimu kwa mfano Sauti ya Mwalimu, kuendesha semina kwa wanachama na viongozi, kutoa mafunzo yanahusu UKIMWI, mafunzo ya ufundishaji bora wa masomo ya Kiingereza, Hisabati, Sayansi na elimu ya mazingira na kuongoza majadiliano katika kuboresha maslahi ya mwalimu nchini. Hata hivyo Chinahova ameiomba Serikali kuendelea kuangalia maslahi bora na kutoa motisha kwa walimu kwani fani ya ualimu ni moja kati ya fani muhimu nchini.
Hamisi Chinahova alisema kuwa walimu wamekuwa wakifanya kazi kwa kujitolea na kwa weledi mkubwa kuhakikisha wanalijenga Taifa hili kwa kuwafundisha wanafunzi kwa juhudi kubwa hivyo Serikali inatakiwa kuangalia upya maslahi yao.
Aidha Chinahova amekumbusha kuwa walimu wamekuwa wakidai madeni mbalimbali ya muda mrefu hivyo wanaiomba Serikali kuhakikisha wanatatua changamoto ya madai ya walimu ili waendelee kufanya kazi ya wito kama awali na hakusita kutoa pongezi kwa Serikali ilivyoboresha mazingira ya kujifunzia.

Sambamba na hilo ameomba watumishi walimu wasipangiwe benki ya kutumia kupitisha mishahara yao kwa kuwa hiyo ni haki ya msingi na Serikali inapaswa kuridhia suala hilo.
Chinahova alimazia kwa kuiomba Serikali kuendelea kuajiri walimu wengi sambamba na ujenzi wa madarasa ili kuwapunguzia changamoto walimu wakiwa kazini na kuahidi wao kama CWT wataendelea kuwakumbusha walimu kutimiza wajibu wao ili iwe rahisi kwa wao kudai maslahi yao.



Kwa habari mbalimbali zinazohusu Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) tafadhali tembelea kurasa zetu za mitandao ya kijamii

**cwt_tz** **chama__cha__walimu__tanzania** **chama cha walimu tanzania**

# Kipendeni Chama kwanza Asema DC Momba



Mkuu wa Wilaya ya Momba Mhe. Fakii Raphael Lulandala (Pichani) amewataka viongozi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) na walimu kwa ujumla kukipenda Chama Cha Walimu kwanza kuliko mtu yeyote na hii itawasaidia wao kuwatetea walimu wanaopata changamoto mbalimbali katika mazingira yao ya kazi kwani hayo ndio majukumu yao na si vinginevyo.

Ameyasema hayo wakati akiongea na viongozi mbalimbali wa CWT mkoani Iringa wakati wa Kongamano la SOHITCO na kuwataka viongozi hao kusimama kidete na kuaminiana wakati wanachama



wao wanapopata matatizo

“Tumekutana hapa kwa sababu ya walimu na tumefahamiana kwa sababu ya CWT hivyo kwa namna yoyote ile hatupaswi kumpenda mtu zaidi ya chama, tukipende chama kwanza mtu baadae, na tusikimbie Chama kisa yule umpendae hayupo. Hivyo ni jukumu letu kumtetea mwalimu kwa gharama yoyote kuliko kitu kingine” Asema Mhe. Lulandala na kuwasisitiza walimu kuendelea kushikamana na kupendana kwani CWT imekuwa mkombozi wa walimu nchini na imesaidia walimu katika matatatizo mbalimbali na hakusita kutoa mifano ya namna gani ambavyo walimu nchini wamekuwa wakinufaika na CWT.

Aidha amewataka walimu nchini kukipenda chama hicho na kuendelea kukiamini kama yeye anavyokiamini kwa kuwa kimekuwa ni msaada mkubwa kwa walimu nchini.




Kwa habari mbalimbali zinazohusu Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) tafadhali tembelea kurasa zetu za mitandao ya kijamii

cwt_tz chama_cha_walimu_tanzania chama cha walimu tanzania

# Benki ya Mwalimu yawa kimbilio Maonesho ya Sabasaba

Benki ya Biashara ya Mwalimu (MCB) imekuwa kimbilio la wananchi wengi katika Maonesho ya Sabasaba ambapo ya watanzania 80 waliotembelea banda la maonesho la benki hiyo walipata mikopo huku wengine zaidi ya 100 wakifungua akaunti.

Mwandishi wetu alipotembelea banda hilo namba 49 kwenye jengo la Jakaya Kikwete, katika maonesho ya 46 ya Biashara maarufu kama Sabasaba alishuhudia umati wa wananchi wakipata huduma kutoka kwa watumishi wa MCB.

Awali kizungumza na waandishi wa habari Julai 7,2022 Mkuu wa Kitengo cha Ukuzaji Biashara na Masoko wa MCB, Leticia Ndongole alisema walitarajia idadi ya wakopaji na wateja wapya ingeongezeka. "Tunaposema huduma tunatoa kwa watu wote maana yake ni walimu, wafanyabiashara, wanafunzi wa vyuo, wakulima, wafugaji, wasafirishaji, vijana na wazee hatuachi mtu.

"Mpaka sasa tumeshawafungulia watu 100 akaunti za aina mbalimbali hivyo tunawakaribisha wote kuja kupata huduma zetu bora kwenye Sekta ya benki.

"Kwetu hii ni mara ya kwanza kushiriki Maonesho haya hakika tumepata mapokezi makubwa kutoka kwa wananchi na tumeona tija yake na tunaahidi kuendelea," alisema Ndongole na kuwataka wananchi baada ya maonesho hayo kuendelea kutembelea matawi ya benki hiyo ya MCB ambapo huduma zilizokuwa zikitolewa Sabasaba zitaendelea kupatikana kwenye matawi hayo.




*Baadhi ya wananchi wakipata huduma kwenye banda la Mwalimu Benki mara baada ya kutembelea banda hilo katika Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.*


# MATUKIO KATIKA PICHA; KONGAMANO LA SOHITCO IRINGA



*Pichani ni viongozi wa CWT kutoka Mkoa Njombe, Mbeya na Rukwa wakiwa katika picha ya pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Iringa Mhe.Mohamed Hassan Moyo (mwenye tai).*



*Wajumbe wa SOHITCO Mkoa wa Iringa kutoka kushoto ni KUT Iringa Mwalimu James Asagwile katikati ni katibu wa Mkoa Hamis Chinahova na kulia ni mwenyekiti wa CWT Mkoa Iringa Stanslaus Mhongole*



*Mwenyekiti wa Chama Cha Walimu mkoa wa Iringa Stanslaus Mhongole akizungumza wakati wa Kongamano la Umoja wa Viongozi wa Chama Cha Walimu Tanzania Kanda ya Nyanda za juu Kusini (SOHITCO)*



*Katibu wa CWT Mkoa Katavi mwalimu Nuru Shenkalwa akizungumza wakati wa Kongamano hilo*



CHAMA CHA WALIMU TANZANIA - CWT
S.L.P 3077 Dodoma. Barua pepe:info@ttu.or.tz Tovuti: www.ttu.or.tz

"CWT kama Chama Cha Wafanyakazi nchini lengo letu kubwa ni kuhakikisha maslahi ya mwalimu tunayatetea na ndio maana kila siku tumekua tukikutana na viongozi wa Serikali uhakikisha hilo linatekelezwa"

#SOHITCO 2022 IRINGA




Mwalimu Dinah Mathamani
Kaimu rais - CWT

cwt_tz chama_cha_walimu_tanzania chama cha walimu tanzania CWT Online TV

CHAMA CHA WALIMU TANZANIA - CWT
S.L.P 3077 Dodoma. Barua pepe:info@ttu.or.tz Tovuti: www.ttu.or.tz

"Tumeamua kuchagua njia ya majadiliano mezani kama njia bora kabisa ya kudai haki na maslahi ya walimu tunaishukuru Serikali imekuwa ikitusikiliza na kutatua changamoto zetu."

#SOHITCO 2022 IRINGA



Mwl. Maganga M. Japhet
Kaimu Katibu Mkuu CWT

cwt_tz chama_cha_walimu_tanzania chama cha walimu tanzania CWT Online TV

CHAMA CHA WALIMU TANZANIA - CWT
S.L.P 3077 Dodoma. Barua pepe:info@ttu.or.tz Tovuti: www.ttu.or.tz

"Niwaombe wanachama wenzangu wa CWT tusemane katika majukwaa sahihi na hii itatusaidia kusimama na kukijenga chama chetu na tusimame imara katika kukitetea Chama hiki.

#SOHITCO 2022 IRINGA#



Protas Magesa
Kaimu Mwekahazina CWT

cwt_tz chama_cha_walimu_tanzania chama cha walimu tanzania CWT Online TV

CHAMA CHA WALIMU TANZANIA - CWT
S.L.P 3077 Dodoma. Barua pepe:info@ttu.or.tz Tovuti: www.ttu.or.tz

Walimu Mkoa wa Iringa tuna imani na RaisSamia Suluhu Hassan na tunamhakikishia tutaendelea kumuunga mkono ili kuhakikisha gururdumu hili la maendeleo ya elimu nchini linasonga mbel.

#SOHITCO 2022 IRINGA#



Mwalimu Stanslaus Mhongole
Mwenyekiti CWT Mkoa Iringa

cwt_tz chama_cha_walimu_tanzania chama cha walimu tanzania CWT Online TV

CHAMA CHA WALIMU TANZANIA - CWT
S.L.P 3077 Dodoma. Barua pepe:info@ttu.or.tz Tovuti: www.ttu.or.tz

Viongozi tushikamane kwa pamoja katika kuhakikisha walimu wanahudumiwa kwa ukaribu kwani Chama hiki ndio kimbilio la Mwalimu katika kutatua changamoto mbalimbali

#SOHITCO 2022 IRINGA#



Mwalimu Nelusigwe Kajuni
Mwenyekiti CWT Mkoa Mbeya.

cwt_tz chama_cha_walimu_tanzania chama cha walimu tanzania CWT Online TV

CHAMA CHA WALIMU TANZANIA - CWT
S.L.P 3077 Dodoma. Barua pepe:info@ttu.or.tz Tovuti: www.ttu.or.tz

Miaka 30 ya maisha ya CWT si mchezo niwaombe walimu itunzeni taasisi hii maana CWT imara ndio uimara wa taaluma ya ualimu nchini.

#SOHITCO 2022 IRINGA#



Mohamed Moyo
Mkuu wa Wilaya Iringa

cwt_tz chama_cha_walimu_tanzania chama cha walimu tanzania CWT Online TV




Kwa taarifa mbalimbali zinazohusu Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) tafadhali tembelea;

# cwt onlive tv

# CWT kuwatetea walimu waliofukuzwa

Mwenyekiti wa Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) Wilayani Geita Mwalimu Samweli Dotto amekiri kupokea taarifa za Kamati ya nidhamu ya Tume ya Utumishi ya walimu wilayani Geita kuwafuta kazi walimu waliorubuniwa na biashara mtandaoni ya Q- NET ambapo ameiomba Serikali kuichunguza kampuni hiyo.

Mwalimu Dotto amesema kazi kubwa ya Chama cha Walimu Tanzania (CWT) ni kuhakikisha kinamtetea mwalimu na kulinda maslahi yake hivyo tumememaliza jukumu hilo na wao kama chama wataendelea na jukumu lao endapo walimu hao wakionyesha ushirikiano kwao.

Akizungumza na waandishi wa habari Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa walimu Wilaya ya Geita, Sitta Mussanga amesema kuwa uamuzi huo umefikiwa na Kamati ya tume hiyo baada ya kufuatilia na kujiridhisha na utoro wa walimu hao uliotokana na wao kuacha kazi na kwenda Q NET ambako waliamini kuna maslahi mazuri zaidi kuliko wajibu wao wa darasani.

Aidha walimu waliofukuzwa ni Kalokola Hurbano na Critus Mkombozi kutoka shule ya sekondari Kivukoni, Stella Ernest wa shule ya msingi Kivukoni, Revocutus Kimasa wa shule ya msingi Mkoani, Aneth Bikombo wa shule ya msingi Nyantorotoro.

Wengine ni Mahemba Peter kutoka shule ya msingi Bukayaga,Benjamini Pertus kutoka shule ya msingi Mtakuja pamoja na Jijaga Galima wa shule ya Msingi Lubanda ambao walishitakiwa na kutuhumiwa kwa nyakati tofauti .

Akiongea kwa niaba ya Chama , Mwenyekiti huyo amesema wanasubiri barua rasmi kutoka kwa walimu hao na baada ya hapo watafuata taratibu kupitia kwa wanasheria wa Chama na kuona namna gani CWT kitawatetea walimu hao katika shauri lao hilo kama wakiamua kukata rufaa.

Walimu hao wanane kutoka Wilaya ya Geita Mkoani Geita wamefukuzwa kazi kwa tuhuma za utoro uliotokana na kujikita kwenye shughuli za kampuni ya mtandao wa biashara maarufu kama Q-NET na kutelekeza majukumu yao ya msingi. Viongozi wa Chama Cha Walimu Tanzania mara kadhaa wamekuwa wakisikika wakiwasihi walimu kutojiingiza katika mikopo au biashara za fedha zinazoweza kuwaletea hasara kubwa huku wakiwashauri wakajiunge katika benki ya Mwalimu ambapo wanaweza kupata huduma mbalimbali zikiwemo za mikopo nafuu.



# Wathibiti ubora ni moyo wa elimu nchini asema Waziri Mkenda

Serikali imekusudia kuimarisha ubora wa elimu nchini ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa inaakisi mahitaji ya watanzania na utandawazi na kasi ya mabadiliko ya teknolojia kwani soko la ajira limezidi kuwa pana hivyo mabadiliko yanahitajika.

Utandawazi huo ni pamoja na watanzania kuchukua fursa ya kufundisha lugha Kiswahili katika vyuo kwenye nchi mbalimbali Duniani.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe Prof. Adolf Mkenda ameyasema hayo tarehe 9 Juni 2022 wakati wa Kikao kazi cha Tathmini ya utendaji kazi idara ya uthibiti ubora wa shule kati ya viongozi, uthibiti ubora wa shule na makao makuu, ithibati ya shule na wathibiti ubora wa shule wakuu Kanda na Wilaya iliyofanyika katika ukumbi wa vijana Jijini Dodoma.

Amewataka wathibiti ubora kote nchini kusimamia kwa weledi zaidi ubora wa elimu kwani wao ni moyo na injini ya elimu.

Amesisitiza umuhimu wa malezi kwenye shule kwani watoto wanaanza shule mapema huku wazazi wakiwa kwenye kinyang'anyiro cha maisha hivyo watoto wanakuwa katika mazingira ambayo hayaakisi ufanisi na nidhamu bora kwa mtoto.

"Tunaona kwenye mitandao mambo ya hovyo yanatokea na sisi tusingependa kupuuza tutakuja na tamko na mikakati baada ya kupitia" Alisema Waziri Mkenda na kuongeza kuwa

"Nyie ni mboni ya elimu hapa nchini, mnapaswa kutunzwa, kuheshimiwa na kulindwa ili elimu iweze kuwa bora, hivyo pambaneni, Serikali imewanunuliwa magari 74 na mambo mengine chungu nzima yanakuja, msichoke"

Waziri Mkenda amesema kuwa Uboreshaji wa elimu kwa kupitia Sera ya elimu ya mwaka 2014 na mapitio ya mitaala sio ajenda ya mtu, hiyo ni agenda ya Serikali ya Tanzania inayoongozwa na Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo maagizo hayo aliyatoa wakati akihutubia Bunge la 12 tarehe 22 Aprili 2021 Jijini Dodoma.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknoloji Prof James Mdoe amempongeza Waziri Mkenda kwa kuwathamini wathibiti ubora kwa kutenga

muda kuhudhuria katika mkutano huo kwani amewaongezea nguvu na ufanisi wa kazi.

Amesema kuwa bila elimu msingi iliyo bora ngazi zingine zote zitakuwa ngumu katika kuthibiti ubora ipasavyo hivyo amewasihi kuongeza weledi kwa ajili ya kazi hiyo.

"Kuna zoezi muhimu sana linaendelea la kupitia mitaala na Sera ya elimu na mafunzo hivyo wathibiti ubora wanapaswa kushiriki kwa kina katika zoezi hilo kwa kiwango kikubwa kwani haitakuwa na maana kama msiposhiriki" Amekaririwa Prof Mdoe.



*Wadau mbalimbali wakifuatilia kikao hicho*


Kwa habari mbalimbali zinazohusu Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) tafadhali tembelea kurasa zetu za mitandao ya kijamii

cwt_tz chama_cha_walimu_tanzania chama cha walimu tanzania

# CWT Pwani walaani ukatili wa kijinsia



Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) Mkoa wa Pwani Kitengo cha Wanawake kimeiomba jamii kutoa ushirikiano kwa vyombo vya sheria pale wanapoona kuna viashiria vya ukatili wa kijinsia. Katibu wa Chama cha Walimu Mkoa wa Pwani, Mwajuma Masenga amesema endapo taarifa hizo zitakuwa zikitolewa mapema zitaleta matokeo chanya katika vita ya kutokomeza vitendo vya ukatili kwa wahusika kudhibitiwa mapema. Ameyasema hayo hivi karibuni Wilayani Kibaha mkoani Pwani kwenye mkutano uliofanyika ukiwa na lengo la kujadili masuala mbalimbali yanayowakabili walimu wanawake wakiwa kazini.

Mwajuma amesema wanalaani vitendo hivyo ambavyo kwa sasa vinaripotiwa katika maeneo mbalimbali, lakini pia wanaiasa jamii kuungana kupiga vita vitendo hivyo visiendelee kutokea.

Naye Katibu wa Wanawake CWT Mkoa wa Pwani, Mwalimu Mariam Mpunga amesema dhumuni lao ni kuhakikisha walimu wanawake wanafanyakazi kwa uadilifu ili kufikia malengo waliyojiwekea ikiwemo kutetea haki zao. Mpunga aliendelea kusema walimu wanawake wana wajibu wa kutetea haki zao wenyewe,lakini pia kuhakikisha wanapambana kwa hali na mali ili kuwalinda wanawake na watoto shuleni na majumbani.




Kumbukumbu Yetu

# Kitengo 'KE' CWT Arusha chawasaidia Watoto

*Machi 07, 2022*

Kitengo cha walimu wanawake cha Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) Mkoa wa Arusha walisherehekea Wiki ya Wanawake kuelekea kilele cha maadhimisho ya Siku ya wanawake Duniani kwa kusaidia mahitaji mbalimbali watoto wenye mahitaji maalum katika shule msingi Patandi.

Akiongea na waandishi wa habari wakati wakitoa misaada hiyo mwenyekiti wa kitengo hicho Mkoa wa Arusha mwalimu Anna Kaaya alisema kuwa wameona washirikiane na watoto wenye mahitaji maalum kwa kuwapelekea mahitaji mbalimbali kama vile sabuni, taulo za kike, mafuta ya kujipaka, sukari na vitu vingine.



# CWT Mbozi wanunua Coaster

***Na Mwandishi wetu, Mbozi***

Uongozi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Wilayani Mbozi Umenunua gari aina ya Coaster kwa lengo la kurahisisha shughuli mbalimbali za kuwahudumia walimu.

Akiongea kwa niaba ya uongozi wa Wilaya hiyo Mwalimu




Kaizer Mjengwa ambaye ni Mwenyekiti wa Chama Cha Walimu wilayani hapa amesema, "Sisi kama Kamati ya uendeshaji na utendaji baada ya kupata wazo kutoka kwa wanachama la kununua gari mapema mwaka 2020 tulianza kutengeneza mipango kwa kushirikisha wawakilishi kutoka shule zaidi ya 225 ambao kwa kauli moja walikubaliana na kupeleka wazo hilo kwenye maeneo yao ya kazi na wakaitisha vikao kisha kwa kauli moja waliamua tununue gari kitu kilichopelekea kurahisisha kazi hiyo" Mjengwa ameongeza pia gari hiyo imenunuliwa kwa lengo la kurahisisha huduma za moja kwa moja kwa wanachama na litakuwa likitumika kwenye shughuli mbalimbali zinazomgusa mwanachama kama vile za maafa na starehe na zile ambazo kwa namna moja au nyingine mwajiri hahusiki kugharamia.

Kwa upande wa mwalimu Yassin Mussa Katibu wa CWT Wilayani Mbozi amesema mpango huu wa ununuzi wa gari ulianza kama wazo na hawakuwa na fedha za kununulia gari hiyo hivyo baada ya taratibu zote kupitia vikao kukamilika fedha zilianza kukusanywa kutokana na marejesho ya asilimia 15 zilizokuwa zinarudi matawini kwa wanachama mpaka pale zilipotimia mapema mwaka huu. "Wanachama waliona ni kwa jinsi gani wanavyohangaika pindi wanapopata majanga,sherehe au safari mbalimbali na wakaona Wilaya zingine nchini wamenunua magari hivyo walikuja na wazo hilo na sisi kama viongozi tukaamua kutekeleza kwa kuwashirikisha wenyewe na wakaamua njia hiyo ndio sahihi inayoweza kutupatia fedha za ununuzi wa gari na tayari gari hilo limeanza kutoa huduma." Amesema Yassin.

CWT Mbozi imekuwa ni Wilaya ya pili Mkoani Songwe kununua gari aina ya Coaster lengo likiwa kurahisisha huduma kwa wanachama wake ambapo gari la awali lilinunuliwa na Wilaya ya Momba.



# CWT Rukwa yawapa walimu magodoro

Uongozi Chama Cha Walimu Tanzania Mkoa wa Rukwa chini ya Mwenyekiti wake Doseph Ndalawa pamoja na Katibu Lazaro Manyama wamekabidhi magodoro 17 kwa Afisa Elimu wa Mkoa wa Rukwa, Komredi Samson Hango ikiwa ni mchango wa Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) kwa walimu wa ajira mpya walioajiriwa na kupangiwa Mkoa wa Rukwa mwezi Julai,2022.

Makabidhiano hayo yalifanyika Juni 8, 2022 katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa ambapo baada ya Afisa Elimu huyo kupokea magodoro hayo aliushukuru uongozi wa CWT Mkoa kwa kitendo hicho kinachoonyesha ukarimu na kuwajali walimu na akawataka wadau wengine kuiga mfano huo mzuri wa Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) ili walimu wanaporipoti katika mkoa husika wajisikie kama wamefika nyumbani.




# CWT Bagamoyo yaendelea kutoa misaada

Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) Wilaya ya Bagamoyo kimeendelea kutoa misaada mbalimbali mashuleni ikiwa ni pamoja na kusaidia vifaa vya ujenzi.

Hatua ya kusaidia vifaa vya ujenzi imekuja baada ya shule ya Sekondari ya Dunda kuezuliwa na upepo kwenye choo cha wanafunzi wa kike na hivyo kufanya wanafunzi hao kupata changamoto ya kupata huduma hiyo muhimu. Vifaa hivyo vilikadhidhiwa hivi karibuni na Mwenyekiti wa CWT Wilaya ya Bagamoyo, Mwl. Hamisi Kimeza pamoja na Katibu wake Mwl. Shaaban Tessua katika viwanja vya shule hiyo.

Katibu Tessua alisema kwamba vifaa hivyo vya upauaji ni hatua ya mwanzo tu ya msaada wao huku vifaa vingine vikiwemo mifuko ya saruji kupitia CWT mkoa wa Pwani kitengo cha walimu wanawake nayo itafuata.

Katika hatua nyingine CWT Wilaya ya Bagamoyo imeendelea kutoa majiko ya gesi kwa ajili ya walimu mashuleni ikiwa ni sehemu ya Mchango wake ili walimu waweze kupata huduma ya pamoja ya chakula wawapo mahalI pa kazi.

Akikabidhi majiko hayo akiwa na baadhi ya wajumbe wa CWT wa kamati ya utendaji ya Wilaya, Mwenyekiti wa Chama hicho Wilaya ya Bagamoyo Mwl. Hamisi Kimeza alisema, lengo la kutoa majiko hayo ni kuongeza mshikamano na upendo kwa walimu wawapo mahali pa kazi, kwani chakula ni eneo mojawapo la kuwakutanisha wote kwa wakati mmoja. Naye Katibu wa Chama hicho Wilaya ya Bagamoyo, alisema kuwa wamefanya zoezi hilo katika awamu mbili kwa baadhi ya shule, lakini lengo ni kuzifikia Shule zote za Halmashauri ya Chalinze pamoja na Bagamoyo zilizopo Wilayani Bagamoyo.



# Walimu nchini wakumbushwa kuzingatia maadili ya kazi



Mkuu wa Wilaya ya Iringa Mohamed Moyo, kwa niaba ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa Queen Sendiga, amewakumbusha walimu kuzingatia maadili yao na kukemea tabia ya baadhi ya walimu ambao wanatia doa taaluma ya ualimu kwa kufanya mapenzi na wanafunzi, jambo ambaolo linachafua taswira ya tasnia hiyo. Alisema hayo wakati akifungua mkutano mkuu wa Umoja wa Viongozi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Nyanda za juu Kusini (SOHITCO)kutoka mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa na katavi.

DC Moyo alisema kuwa wapo baadhi ya walimu wanadiriki kufanya mapenzi na watoto wadogo kinyume na maadili ya utumishi wa umma na kuchafua taswira nzima ya tasnia ya ualimu.

Aidha, ameomba viongozi wote kuungana pamoja kukemea jambo hilo kwa kada ya ualimu, kwani kada hiyo ni nyeti ambayo kila mtu lazima apitie katika mkono wa mwalimu.

“”Mimi leo hii nisingekuwa Mkuu wa Wilaya bila kufundishwa na mwalimu, nimefundishwa na mwalimu ndio maana Serikali imeniamini na kuniteuwa kuwa Mkuu wa Wilaya kutokana na mwalimu,” alisema Moyo. Alisema kuwa walimu wanadhima kubwa ya kuweka maadili mema ya watoto wanaowafundisha,

hivyo basi, walimu wasijiingize katika tamaa ya kufanya mapenzi na watoto huo ni ukatili dhidi ya watoto. Moyo aliwataka viongozi kuweka mshikamano na kuwashughulikia wale wote wanajihusisha na masuala ya mapenzi na wanafunzi kuhakikisha hatua za kinidhamu zinachukuliwa.

Kwa upande wa changamoto ya upungufu wa walimu mashuleni, alisema kuwa Serikali inaendelea kuajiri walimu kadiri inavyowezekana ili kupunguza changamoto ya uhaba wa walimu sambamba na kuboresha miundombinu ya shule.

“Serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassani inaonesha nia ya kuboresha Sekta ya elimu kwa kutambua jitihada inayofanywa na walimu na kwamba Serikali itaendelea kushirikiana na Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) kuhakikisha kwamba sekta ya elimu inaboreshwa,” aliongeza.

Alisema kuwa Serikali inatambua changamoto ambazo walimu wanakabiliana nazo lakini bado wanafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kwamba watoto wanafanya vizuri pamoja na kufaulu mitihani yao.



Sauti ya Mwalimu

CHAMA CHA WALIMU TANZANIA
CWT
WAJIBU NA HAKI

Toleo Na.006 Agosti - Septemba 30, 2022

Baadhi ya Wajumbe na Walimu waliohudhuria Kongamano la SOHITCO lililofanyika Iringa lililojumuisha Mikoa sita ya Iringa, Mbeya, Njombe, Songwe, Rukwa na Katavi wakiwa katika picha ya pamoja



